# SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR YA 2016

## MPANGILIO WA VIFUNGU


| VIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| | **SEHEMU YA KWANZA**<br>**UTANGULIZI** |
| 1. | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| 2. | Kusomwa. |
| | **SEHEMU YA PILI**<br>**VIFUNGU VYA MAREKEBISHO** |
| 3. | Marekebisho ya kifungu cha 2. |
| 4. | Marekebisho ya kifungu cha 12. |
| 5. | Kufuta kifungu cha 14. |
| 6. | Marekebisho ya kifungu cha 16. |
| 7. | Kuongeza kifungu kipya 16A. |
| 8. | Kuongeza kifungu kipya 16B. |
| 9. | Kuongeza kifungu kipya 16C. |
| 10. | Kuongeza kifungu kipya 16D. |
| 11. | Marekebisho ya kifungu cha 20. |
| 12. | Marekebisho ya kifungu cha 21. |
| 13. | Kuongeza kifungu kipya 24A. |
| 14. | Kuongeza kifungu kipya 24B. |
| 15. | Kuongeza kifungu kipya 24C. |
| 16. | Kuongeza kifungu kipya 24D. |
| 17. | Kuongeza kifungu kipya 24E. |
| 18. | Marekebisho ya kifungu cha 26. |
| 19. | Kuongeza kifungu kipya 26A. |
| 20. | Kuongeza kifungu kipya 26B. |
| 21. | Kuongeza kifungu kipya 28A. |
| 22. | Kuongeza kifungu kipya 29A. |
| 23. | Kuongeza kifungu kipya 29B. |
| 24. | Kuongeza kifungu kipya 36A. |
| 25. | Marekebisho ya Kifungu cha 56. |
| 26. | Marekebisho ya kifungu cha 57. |

**SHERIA NAM 7 YA 2016**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

19th October, 2016

# SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR, NAM. 8 YA 1999 KAMA ILIVYOREKEBISHWA NA SHERIA NAM. 11 YA 2009 NA KUWEKA MASHARTI BORA PAMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Marekebisho) ya 2016 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Kusomwa.

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Nam. 8 ya 1999 kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam.11ya 2009 ambapo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria mama".

## SEHEMU YA PILI
## VIFUNGU VYA MAREKEBISHO

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**3.** Kifungu cha 2 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno yafuatayo:

(a) "Wakuu Wasaidizi wa Skuli" na "Wakurugenzi Wasaidizi" maana yake ni Wasaidizi Wakuu wa Wakuu wa Skuli au Wakurugenzi Wasaidizi wa Wakurugenzi;

(b) "Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu" maana yake ni Bodi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria hii;

(c) "Wafanyakazi Wataalamu" maana yake ni Wafanyakazi Wataalamu wa Chuo Kikuu kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria hii.

Marekebisho ya kifungu cha 12.

**4.** Kifungu cha 12 (1)(d) cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(i) kwa kuondosha maneno "si chini ya wanane na si zaidi ya kumi na moja" na kuweka badala yake maneno "si zaidi ya kumi na sita".

(ii) kwa kuongeza kipengele xi, xii, xiii na xiv katika orodha iliopo:

(xi) mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na Afya;

(xii) mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na Utalii;

(xiii) mjumbe mmoja kutoka Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar;

(xiv) mjumbe mmoja ambae ni muwakilishi wa Jumuiya ya Wafanyakazi wa Uendeshaji na Wataalamu wa Chuo.

(iii) kwa kufuta neno "tatu" lililopo katika Kifungu cha 12(1)(d)(iv) cha Sheria mama na kuweka badala yake neno "moja."

Kufuta kifungu cha 14.

**5.** Kifungu cha 14 cha Sheria mama kama kilivyorekebishwa na kifungu cha 7 cha Sheria Nam. 11 ya 2009 kinafutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**6.** Kifungu cha 16 cha Sheria mama kinafutwa na kuwekwa kifungu chengine badala yake kama ifuatavyo:

Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu.

16.(1) Kutakuwa na Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Makamu Mkuu wa Chuo ambae atakuwa Mwenyekiti;

(b) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayehusika na Taaluma, Utafiti na Ushauri elekezi ambae atakuwa Makamu Mwenyekiti;

(c) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayehusika na Mipango, Fedha na Utawala ambae atakuwa ni Katibu;

(d) Mkuu wa Skuli mmoja anaeteuliwa na Makamu Mkuu wa Chuo;

(e) Mkurugenzi mmoja anaeteuliwa na Makamu Mkuu wa Chuo;

(f) Wajumbe wawili wanaoteuliwa na Baraza kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza ambapo mmoja miongoni mwao ni mwanamke;

(g) Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu; na

(h) Mjumbe mmoja kutoka Chama cha Wafanyakazi katika Chuo.

(2) Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu, kwa maoni yake, inaweza kualika mtu, au watu wengine ambao wanaweza kurahisisha kufikia maamuzi sahihi ya Bodi.

(3) Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu itakuwa na kazi zifuatazo kwa mujibu wa uwezo ilionao chini ya Sheria hii au kazi itakayopewa na Baraza:

(a) kuandaa orodha ya nafasi zilizo wazi kwa kila mwaka kwa ajili ya kuidhinishwa na Baraza;

(b) kuthibitisha ajira za wafanyakazi wapya kama itakavyopewa kazi hiyo na Baraza;

(c) kupendekeza ajira za wafanyakazi wapya kwa ajili ya kupata idhini ya Baraza;

(d) kuzingatia na kupendekeza maslahi na mishahara ya wafanyakazi;

(e) kuzingatia na kutoa mapendekezo ya upandishaji vyeo kwa wafanyakazi wanataaluma na Uendeshaji au kada nyengine yoyote; na

(f) kupendekeza na kusimamia shughuli za mafunzo ya wafanyakazi wa Chuo kwa kila mwaka wa fedha.

(4) Masharti yaliyomo katika Jadweli la kwanza la Sheria mama yatatumika sambamba kuhusiana na muda wa utumishi na vikao kwa wajumbe wa Bodi ya Ajira na Raslimali Watu.

Kuongeza kifungu kipya 16A.

**7.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 16A kama ifuatavyo:

Kamati ya Ajira na Rasilimali Watu.

16A.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Ajira na Rasilimali Watu katika kila Skuli au Taasisi ya Chuo kwa kadri Baraza litakavyoona inafaa, ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkuu wa Skuli husika ambae atakuwa Mwenyekiti;

(b) Afisa dhamana wa Kitengo cha Rasilimali Watu katika Skuli husika ambae atakuwa Katibu;

(c) Mkuu Msaidizi wa Skuli;

(d) Wakuu wa Idara za Taaluma; na

(e) Mjumbe mmoja kutoka Chama cha Wafanyakazi katika Skuli au Taasisi husika ya Chuo.

(2) Kamati ya Ajira na Rasilimali Watu, kwa maoni yake, inaweza kumualika mtu yeyote au watu ambao watarahisisha kufikia maamuzi sahihi ya Kamati.

(3) Kamati ya Ajira na Rasilimali Watu itafanya kazi mahususi au kazi nyenginezo itakayopewa na Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu.

Kuongeza kifungu kipya 16B.

**8.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 16B kama ifuatavyo:

Bodi ya Fedha, Mipango na Maendeleo.

16B.-(1)Kutakuwa na Bodi ya Fedha, Mipango na Maendeleo ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Baraza kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza ambapo mmoja wao atakuwa Mwenyekiti wa Bodi; wakati wa uteuzi huo, Baraza litazingatia jinsia;

(b) Makamu Mkuu wa Chuo;

(c) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayehusika na Mipango, Fedha na Uendeshaji ambaye ni Katibu;

(d) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayehusika na Taaluma, Utafiti na Ushauri elekezi;

(e) Msarifu; na

(f) Mkuu wa Idara ya Mipango.

(2) Bodi ya Fedha, Mipango na Maendeleo itafanya kazi kama itakavyopewa na Baraza kama ifuatavyo:

(a) kusimamia mipango ya fedha ya Chuo Kikuu na kulishauri Baraza kuhusu masuala yoyote yanayohusiana na usimamizi wa fedha;

(b) kuweka kumbukumbu zote za mahesabu katika utaratibu unaokubaliwa na Serikali zinazohusiana na mapato na matumizi ya Chuo;

(c) kuandaa ripoti za fedha za robo mwaka na za mwaka na kuziwasilisha katika Baraza;

(d) kufatilia utekelezaji sahihi wa kanuni za fedha na Sheria ya Manunuzi;

(e) kuandaa, kufatilia na kuweka pamoja Bajeti ya Chuo Kikuu na kuiwasilisha katika Baraza;

(f) kupendekeza mipango na miradi ya uwekezaji kwa ajili ya idhini ya Baraza;

(g) kufatilia na kuandaa ripoti ya robo mwaka ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Skuli na Taasisi ya Chuo;

(h) kuandaa na kuwasilisha taarifa na mapendekezo yanayohusiana na masuala ya fedha kwa Baraza;

(i) kusimamia Bajeti na masuala yote ya fedha kwa kila Skuli ya Chuo; na

(j) kuandaa ripoti ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

(3) Masharti yaliyomo katika Jadweli la Kwanza la Sheria mama yatatumika sambamba kuhusiana na muda wa utumishi wa wajumbe wa Bodi ya Fedha, Mipango na Maendeleo.

Kuongeza kifungu kipya 16C.

**9.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 16C kama ifuatavyo:

Kamati ya Fedha, Mipango na Maendeleo.

16C.-(1) Kutaanzishwa Kamati ya Fedha katika kila Skuli au Taasisi kama ambavyo Baraza litaona inafaa, ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkuu wa Skuli au Taasisi husika atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mkuu Msaidizi wa Skuli au Taasisi; na

(c) Afisa dhamana wa Kitengo cha Fedha.

(2) Kamati ya Fedha itakuwa na kazi mahususi na kazi nyengine kama itakavyopewa na Bodi ya Fedha, Mipango na Maendeleo.

(3) Baraza litaandaa na kuidhinisha Kanuni zinazohusiana na Uendeshaji wa Vitengo na Kamati zote za Chuo.

Kuongeza kifungu kipya 16D.

**10.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 16D kama ifuatavyo:

Bodi ya ustawi wa wanafunzi.

16D.-(1)Kutakuwa na Bodi ya Ustawi wa Wanafunzi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambae atateuliwa na Baraza kutoka miongoni mwa wajumbe wake ambao si wajumbe kwa nafasi zao;

(b) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayehusika na Taaluma, Utafiti na Ushauri elekezi;

(c) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anaehusika na Mipango,Fedha na Uendeshaji;

(d) Mwakilishi mmoja wa wanafunzi kutoka katika Baraza la Chuo Kikuu;

(e) Mkuu wa Ustawi wa Wanafunzi, ambae atakuwa pia ni Katibu;

(f) Mwakilishi kutoka Seneti,

(g) Mwakilishi wa Wanafunzi wa Shahada za juu; na

(h) Wawakilishi wawili wa wanafunzi angalau mwanamke mmoja kutoka Jumuiya ya Wanafunzi.

(2) Bodi ya Ustawi wa Wanafunzi itakuwa na kazi kwa kadri itakavyopewa na Baraza.

(3) Masharti yaliyomo katika Jadweli la kwanza la Sheria mama yatatumika sambamba kuhusiana na muda wa utumishi kwa wajumbe wa Bodi ya Ustawi wa Wanafunzi.

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**11.** Kifungu cha 20(2) (b) cha Sheria mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kama ifuatavyo:

(b) Taasisi ya Maendeleo ya Utalii; na

(c) Taasisi ya Taaluma za Baharini.

Marekebisho ya kifungu cha 21.

**12.** Kifungu cha 21 cha Sheria mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo:

Kamati ya Taaluma.

21.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Taaluma katika kila Skuli au Taasisi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkuu wa Skuli husika ambae atakuwa Mwenyekiti;

(b) Msaidizi Mkuu wa Skuli au Taasisi;

(c) Wakuu wa Idara za Taaluma;

(d) Mjumbe mmoja anaeteuliwa na Seneti kutoka nje ya Chuo ambae atakuwa na sifa ya Taaluma husika; na

(e) Wajumbe wawili wanaochaguliwa na wanafunzi kutoka katika Skuli husika ambapo angalau mmoja atakuwa mwanamke.

(2) Kila Kamati ya Taaluma kwa kuzingatia masharti makhsusi na masharti ya jumla ya Seneti italazimika kufanya kazi zifuatazo:

(a) kusimamia elimu, ufundishaji na utafiti ndani ya Skuli;

(b) kutoa mapendekezo kwa Seneti kuhusiana na jambo lolote la kitaaluma linalohusu Skuli; na

(c) kufanya jambo au kitu chochote itakayopewa uwezo wa kufanya na Seneti au kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(3) Kamati ya Taaluma, kwa maoni yake, inaweza kumualika mtu yeyote au watu ambao watarahisisha kufikia maamuzi sahihi ya Kamati.

(4) Masharti ya Jadweli ya Kwanza ya Sheria mama yatatumika sambamba kuhusiana na muda wa Utumishi na vikao vya Wajumbe wa Kamati ya Taaluma.

Kuongeza kifungu kipya 24A.

**13.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 24A kama ifuatavyo:

Wakuu Wasaidizi wa Skuli na Wakurugenzi Wasaidizi

24A.-(1)Kutakuwa na:

(a) Wakuu Wasaidizi wa kila Skuli; na

(b) Mkurugenzi Msaidizi wa kila Taasisi ya Chuo kwa kadri itakavyoamuliwa na Baraza kutokana na ushauri wa Seneti.

(2) Mkuu Msaidizi wa Skuli au Mkurugenzi Msaidizi atakuwa ni msaidizi wa Mkuu wa Skuli au Msaidizi wa Mkurugenzi, kama hali itavyokuwa, na atakaimu nafasi ya Mkuu wa Skuli au Mkurugenzi atakapokuwa hayupo au nafasi ya Mkuu wa Skuli au Mkurugenzi itakapokuwa tupu.

(3) Mkuu Msaidizi wa Skuli au Mkurugenzi Msaidizi atakuwa Msaidizi Mkuu na atawajibika kwa Mkuu wa Skuli au Taasisi katika mambo yote yanayohusiana na shughuli na maisha ya Skuli, Taasisi na Chuo kwa ujumla.

(4) Mkuu Msaidizi wa Skuli au Mkurugenzi Msaidizi atafanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria mama kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam. 11 ya 2009 na Sheria hii au kama atakavyoelekezwa na Baraza.

Kuongeza kifungu kipya 24B.

**14.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 24B kama ifuatavyo:

Sifa za Mkuu wa Skuli au Mkurugenzi.

24B. Mtu atasitahiki kuteuliwa kuwa Mkuu wa Skuli au Mkurugenzi endapo:

(a) atakuwa na shahada ya Uzamivu au Mhadhiri Mwandamizi; na

(b) atakuwa na uzoefu angalau miaka mitatu ya kazi za utawala katika Taasisi za Elimu ya Juu zinazotambulika na Serikali ya Mapinduzi.

Kuongeza kifungu kipya 24C.

**15.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 24C kama ifuatavyo:

Uteuzi wa Mkuu Msaidizi wa Skuli au Mkurugenzi Msaidizi.

24C-(1) Mkuu Msaidizi wa Skuli au Mkurugenzi Msaidizi atateuliwa na Baraza kwa mujibu wa Kanuni zitakazotungwa na Baraza.

(2) Mtu atasitahiki kuteuliwa kuwa Mkuu Msaidizi wa Skuli au Mkurugenzi Msaidizi endapo:

(a) atakuwa angalau na Shahada ya Uzamili; na

(b) atakuwa na uzoefu angalau miaka mitatu ya kazi za utawala katika Taasisi ya elimu inayotambulika.

(3) Mkuu Msaidizi wa Skuli au Mkurugenzi Msaidizi atashika wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wake na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu cha miaka mitatu.

Kuongeza kifungu kipya 24D.

**16.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 24D kama ifuatavyo:

Idara na Vituo vya Taaluma na Uendeshaji.

24D.-(1) Kutakuwa na Idara na Vituo vya Taaluma na Uendeshaji katika Chuo kama vitakavyoanzishwa na Baraza.

(2) Makamu Mkuu wa Chuo atawateuwa Wakuu wa Idara na Vituo baada ya kushauriana na Manaibu Makamu Wakuu wa Chuo, na Mkuu wa Skuli au Mkurugenzi wa Skuli au Taasisi husika.

(3) Makamu Mkuu wa Chuo atawateuwa Wakuu wa Idara na Vituo vya Uendeshaji kwa kushauriana na Naibu Makamu Wakuu wa Chuo.

(4) Wakuu wa Idara za Taaluma na Uendeshaji watateuliwa kutoka miongoni mwa wafanyakazi waandamizi wa Chuo kupitia taratibu za Baraza.

(5) Wakuu wa Idara za Taaluma na Uendeshaji watashikilia nafasi zao kwa muda wa miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja chengine cha miaka mitatu.

(6) Makamu Mkuu wa Chuo anaweza, baada ya kushauriana na Naibu Makamu Wakuu wa Chuo, kuteuwa Wakuu Wasaidizi wa Idara kuwasaidia Wakuu wa Idara kama atakavyoona inafaa kwa mujibu wa taratibu zitakazotungwa na Baraza.

(7) Baraza litatunga Kanuni zitakazotoa muongozo wa uteuzi wa Wakuu wa Idara za Taaluma na uendeshaji.

Kuongeza kifungu kipya 24E

**17.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 24E kama ifuatavyo:

Kazi na Wajibu.

24E. Pamoja na kazi na majukumu mengine, Wakuu wa Idara za Taaluma na Uendeshaji:

(a) wataongoza mikutano ya Idara zao;

(b) watawakilisha Idara zao katika Kamati za Chuo na vyombo vyengine kama itavyohitajika;

(c) watahakikisha viwango bora vya utafiti na ushauri elekezi, ufundishaji, kujifunza na utumishi wa umma vinaendelea;

(d) wataongoza kitaalamu na kuwajibika katika uendeshaji wa Idara zao;

(e) wataweka kumbukumbu sahihi za Idara zao na zinazoenda na wakati; na

(f) watasimamia watendaji katika Idara zao.

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**18.** Kifungu cha 26 cha Sheria mama kinafutwa na kuwekwa badala yake ifuatavyo:

Vitengo vya Uendeshaji vya Skuli.

26.-(1) Kutakuwa na Kitengo au Vitengo vya Uendeshaji kwa kila Skuli au Taasisi ya Chuo kama ambavyo Baraza litaona inafaa.

(2) Kitengo cha uendeshaji kitaongozwa na Afisa Dhamana na ambae atateuliwa na Mkuu wa Skuli au Mkurugenzi wa Taasisi baada ya kupokea mapendekezo ya Kamati ya Ajira ya Skuli au Taasisi husika.

(3) Baraza litatunga Kanuni za Uendeshaji wa Vitengo katika Chuo.

(4) Wafanyakazi wa Uendeshaji watajumuisha wafuatao:

(a) Mkuu wa Ustawi wa Wanafunzi;

(b) Msarifu;

(c) Watendaji wa Chuo wanaofanya kazi za uendeshaji kama ambavyo muda baada ya muda Baraza litaamua; na

(d) Watendaji wengine wa Chuo wenye kazi nyengine zisizohusiana na ufundishaji, utafiti, ushauri elekezi au uvumbuzi kama ambavyo Baraza litaamua kwa kushauriana au kwa mapendekezo ya Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu.

Kuongeza kifungu kipya 26A.

**19.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 26A kama ifuatavyo:

Watendaji Wataalamu wa Chuo.

26A-(1) Watendaji wataalamu wa Chuo watajumuisha wafuatao:

(a) Wafanyakazi wa Afya na Tiba;

(b) Wahandisi, wasanifu majengo, watathimini ujenzi na wataalamu wengine wa fani zinazohusiana na hizo;

(c) Wanasayansi wa maabara;

(d) Wataalamu wa Teknolojia na wasimamizi wa mifumo ya habari;

(e) Mafundi; na

(f) Mafundi wengine kama Baraza litakavyoona inafaa kuwaongeza.

(2) Uwezo wa kuteuwa wafanyakazi wataalamu utakuwa ni wa Baraza.

(3) Kada za wafanyakazi Wataalamu watateuliwa na Baraza kwa mapendekezo ya Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu na kwa mujibu wa miongozo inayotolewa kila baada ya muda.

Kuongeza kifungu kipya 26B.

**20**. Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 26B kama ifuatavyo:

Jumuiya ya wafanyakazi wa Uendeshaji na Wataalam.

26B-(1) Kutakuwa na Jumuiya ya wafanyakazi wa Uendeshaji na Wataalamu ambayo itajumuisha wafanyakazi ambao sio Wanataaluma pamoja na mwanachama mmoja kutoka katika Chama cha Wafanyakazi wa Chuo.

(2) Baraza linaweza kuidhinisha kuanzishwa na kufutwa kwa Jumuiya yoyote ya wafanyakazi kama litakavyoona inafaa kwa kupokea maombi na Katiba ya wafanyakazi wanaokusudia kuunda Jumuiya ndani ya Chuo pamoja na malengo ambayo hayapingani na malengo ya Chuo na masharti ya Sheria nyengine.

(3) Kazi za Jumuiya zitasimamiwa kwa mujibu wa Katiba zao ambazo zitaidhinishwa na Baraza ikijumuisha marekebisho yake.

Kuongeza kifungu kipya 28A.

**21.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 28A kama ifuatavyo:

Katibu wa Baraza.

28A.-(1) Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Chuo ambaye atateuliwa na Baraza kutoka miongoni mwa Maafisa Sheria Waandamizi wa Chuo baada ya kupokea mapendekezo ya Bodi ya Ajira na Rasilimali Watu kwa kuzingatia miongozo na masharti yaliyowekwa na Baraza.

(2) Katibu wa Baraza atawajibika kwa Baraza, na atakuwa na kazi za kuhakikisha kwamba:

(a) taarifa za mikutano zinatolewa kwa wakati;

(b) kumbukumbu za mikutano ya Baraza zinachukuliwa na kuhifadhiwa kwa usahihi;

(c) maagizo na maelekezo ya Baraza yanatekelezwa kwa ukamilifu;

(d) anatoa ushauri kwa Baraza kila inapohitajika; na

(e) kusimamia na kutekeleza kazi kwa kadiri atakavyopangiwa na Baraza.

(3) Baraza linaweza pia kuwateuwa maafisa kadhaa kwa ajili ya kumsaidia katibu kwa kadri Baraza litakavyoona inafaa.

(4) Katibu wa Baraza la Chuo atakuwa na haki ya kuhudhuria vikao vyote vya Baraza lakini hatakuwa na haki ya kupiga kura.

(5) Katibu wa Baraza atakuwa ni Mkuu wa Sekretarieti ya Baraza na Idara ya Huduma za Sheria ya Chuo.

Kuongeza kifungu kipya 29A.

**22.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 29A kama ifuatavyo:

Kamati ya nidhamu kwa wafanyakazi.

29A.(1) Kutakuwa na Kamati ya Nidhamu kwa wafanyakazi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Baraza kutoka miongoni mwa wajumbe wake, ambapo mmoja miongoni mwao atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;

(b) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anaehusika na Mipango, Fedha na Uendeshaji;

(c) Mwakilishi kutoka:

(i) Jumuiya ya wafanyakazi wa Taaluma wa Chuo atakae teuliwa na Makamu Mkuu wa Chuo baada ya kushauriana na Jumuiya ya wafanyakazi wa Taaluma.

(ii) Jumuiya ya wafanyakazi wa Uendeshaji na Wataalamu.

(iii) Chama cha Wafanyakazi katika Chuo.

(d) Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu;

(e) Mkuu wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu za Chuo; na

(f) Afisa Sheria Mwandamizi kutoka katika Chuo, na ambaye atakuwa pia Katibu.

(2) Akidi ya vikao vya Kamati ya Nidhamu kwa Wafanyakazi itakuwa uwepo wa angalau wajumbe watano.

(3) Mashtaka ya makosa ya kinidhamu au ukiukwaji wa maadili ya kazi dhidi ya mfanyakazi yatashughulikiwa kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria mama na mapendekezo yatawasilishwa katika Baraza kupitia Makamu Mkuu wa Chuo.

(4) Mambo yote yanayohusiana na nidhamu kwa wafanyakazi; isipokuwa kwa Makamu Mkuu wa Chuo na Naibu Makamu Wakuu wa Chuo yatashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria hii au Sheria nyengine zilizopo Zanzibar.

(5) Kamati ya Nidhamu kwa Wafanyakazi itaongozwa na Sheria hii, Sheria ya Utumishi wa Umma au Sheria nyengine zozote zinazotumika Zanzibar.

(6) Baraza linaweza kutunga Kanuni kuhakikisha nidhamu miongoni mwa wafanyakazi wa Chuo.

Kuongeza kifungu kipya 29B.

**23.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 29B kama ifuatavyo:

Kamati ya Rufaa ya Wafanyakazi.

29B.-(1) Kunaanzishwa Kamati inayojulikana kama Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wafanyakazi ambayo itashughulikia Rufaa za wafanyakazi wa Taaluma, Uendeshaji na Wataalamu.

(2) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wafanyakazi itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Mjumbe mmoja kutoka Kamisheni ya Utumishi wa Umma atakaeteuliwa na Baraza kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma na ambae atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa Vyuo Vikuu vilivyopo Zanzibar atakaeteuliwa na Baraza kwa kushauriana na Makamu Mkuu wa Chuo husika;

(c) Wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu atakaeteuliwa na Makamu Mkuu wa Chuo baada ya kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(d) Mjumbe mmoja atakaeteuliwa na Makamu Mkuu wa Chuo kutoka miongoni mwa Maafisa Waandamizi wa Uendeshaji ambae atakuwa Katibu.

(3) Wajumbe wa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wafanyakazi watateuliwa pale ambapo shauri la kinidhamu linapotokea.

(4) Akidi ya Kikao cha Kamati ya Rufaa ya Nidhamu itakuwa ni zaidi ya nusu ya Wajumbe wa Kamati;

(5) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wafanyakazi itakuwa na uwezo wa kusikiliza na kuamua maamuzi yoyote yanayohusiana na nidhamu, kufukuzwa na kuachishwa kazi katika Chuo.

(6) Kamati ya rufaa ya nidhamu itaendesha shughuli zake kwa mujibu wa Sheria hii, Sheria ya Utumishi wa Umma, au Sheria yoyote inayotumika Zanzibar.

(7) Maamuzi ya Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wafanyakazi chini ya kifungu hiki yatakuwa ni ya mwisho katika ngazi ya Chuo.

Kuongeza kifungu kipya 36A.

**24.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 36A kama ifuatavyo:

Chuo Kikuu kinacho-jitegemea.

36A. Mkuu wa Chuo anaweza, kwa ushauri wa Baraza, kutoa amri kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali, kutangaza Chuo Kishiriki, Skuli au Taasisi ya Chuo kuwa Chuo Kikuu kinachojitegemea.

Marekebisho ya Kifungu cha 56.

**25.** Kifungu cha 56 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kijifungu cha 56 (1) (o) kama ifuatavyo:

56(1)(o) zitakazoeleza mgawanyo, usimamizi, udhibiti na matumizi ya fedha kwa Makamu Mkuu, Manaibu Makamu Wakuu, Wakuu wa Skuli, Wakurugenzi wa Taasisi na Maafisa wengine wa Chuo.

Marekebisho ya kifungu cha 57

**26.** Sheria mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 57 na kuweka kifungu kipya cha 57 kama ifuatavyo:

Kufuta na kubakiza.

**57.**(1) Sheria zifuatazo zinafutwa:

(a) Sheria ya Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Namba 4 ya mwaka 1979;

(b) Sheria ya Chuo cha Afya Zanzibar, Nam.10 ya 1998,

(c) Sheria ya Taasisi ya Usimamizi wa Fedha, Nam.1 ya 2002, na

(d) Sheria ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii Nam. 7 ya 2008.

(2) Bila ya kuathiri kufutwa kwa Sheria zilizoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, amri zote, teuzi, ajira, kanuni, au jambo lolote lilofanywa chini ya Sheria zilizofutwa, litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria mama kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam. 11 ya 2009 na Sheria hii.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni za udahili wa Chuo Kikuu cha Taifa Cha Zanzibar, wanafunzi wote waliodahiliwa kwa Sheria zilizofutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watahitimu mafunzo yao kwa kutunukiwa vyeti vyenye majina ya Taasisi zilizowadahili mwanzoni na kusainiwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Taasisi zilizofutwa chini ya kifungu hiki.

**Umepitishwa** na Baraza la Wawakilishi, tarehe 28 Septemba, 2016.

**{RAYA ISSA MSELLEM}**
**KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**